



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU UCHAGUZI MDOGO JIMBO LA AMANI - ZANZIBAR

Zanzibar, 15 Disemba, 2022

Kwa mujibu wa ibara ya 74(6)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Tume ina wajibu wa kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kifungu cha 37 (1) na (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi sura ya 343, Tume ina jukumu la kuendesha chaguzi ndogo za ubunge inapotokea nafasi wazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kifo.

Kwa kuzingatia masharti ya vifungu vya 7 na 8 vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume huteua watendaji mbalimbali wa uchaguzi kwa ajili ya kuendesha na kusimamia zoezi la uchaguzi. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, utaratibu wa upatikanaji wa watendaji wa uchaguzi unahusisha mchakato wa upatikanaji wa ajira za muda za watumishi wa umma kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uchaguzi. Watendaji hao ni Msimamizi wa Uchaguzi (RO) na msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya Jimbo (ARO Jimbo).

Ili kupata watu wenye sifa stahiki Tume ilitoa tangazo la ajira za muda kwa nafasi ya Msimamizi wa Uchaguzi mmoja na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi wawili. Tangazo hilo lilitolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii na lilikaribisha maombi ya ajira za muda za watumishi wa umma wenye sifa za kujaza nafasi ya Msimamizi wa Uchaguzi na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi katika Jimbo la Amani, Wilaya ya Mjini, Zanzibar.

Tangazo lililotolewa lilielekeza watumishi wa umma raia wa Tanzania, wenye stahahada, stahahada ya juu au shahada katika fani mbalimbali kuwasilisha maombi yao kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi kuanzia tarehe 04 -10 Novemba, 2022.

Usaili ulifanyika tarehe 14 Novemba, 2022 na waombaji 3 waliofaulu usaili kwa alama za juu waliteuliwa na Tume katika kikao chake cha tarehe 14 Novemba, 2022, mmoja

kuwa Msimamizi wa Uchaguzi (RO) na wawili kuwa Wasimamizi Wasaidizi ngazi ya Jimbo (ARO Jimbo).

Watendaji hao walipewa Ofisi za muda kwa ajili ya kuratibu na Kusimamia Uchaguzi katika eneo la Saateni (Kwa Abass Hussein) yalipo maghala ya Tume kwa ajili ya kukamilisha zoezi la kusimamia uchaguzi kama ajira zao za muda zinavyoelekeza.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi NEC ina Ofisi zake za kudumu eneo la Maisara ambapo vyama vya siasa, wapiga kura, wananchi na wadau mbalimbali hufika kupata huduma za kiofisi. Kuhusu masuala ya Uchaguzi Majimboni, Tume hutafuta ofisi za muda kwa watendaji wa muda walioajiriwa kusimamia chaguzi hizo.

Kwa mujibu wa ibara ya 74(13) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii, Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano itashauriana mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi ya Tanzania Zanzibar.

Aidha, kifungu cha 12A (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura 343, kinaeleza kuwa; Bila kujali masharti ya kifungu cha 12, kwa madhumuni ya uendeshaji wa uchaguzi wa Wabunge na Rais Tanzania Zanzibar, sheria inayohusu uandikishaji wa wapiga kura na daftari la wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, itakuwa ndiyo sheria ya uandikishaji wa wapiga kura na daftari la wapiga kura Tanzania Zanzibar kwa madhumuni ya Sheria hii, na

Vilevile, kifungu cha 12A (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura 343, kinaeleza kuwa; Tume itamwandikisha mtu yeyote aliyepo Tanzania Zanzibar ambaye anastahili tu kuandikishwa kuwa mpiga kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Hivyo Tume inawakumbusha wananchi wa Jimbo la Amani kujitokeza kushiriki Uchaguzi mdogo wa Jimbo la Amani utakaofanyika siku ya Jumamosi tarehe 17 Disemba, 2022 ili kutimiza haki yao ya Kikatiba ya kuchagua Mgombea wanayemtaka kwa nafasi ya Ubunge.



Adam Mkina

Kny: MKURUGENZI WA UCHAGUZI
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI